# YESU NI NANI?

UJIO MWAKA
YOHANA 1:1-5



'HAPO MWANZO KULIKUWAPO NENO, NAYE NENO ALIKUWAPO KWA MUNGU, NAYE NENO ALIKUWA MUNGU. HUYO MWANZO ALIKUWAKO KWA MUNGU. VYOTE VILIFANYIKA KWA HUYO, WALA PASIPO YEYE HAKIKUFANYIKA CHO CHOTE KILICHOFANYIKA. NDANI YAKE NDIMO ULIMOKUWA UZIMA, NAO ULE UZIMA ULIKUWA NURU YA WATU. NAYO NURU YANG'AA GIZANI, WALA GIZA HALIKUIWEZA. ' (YOHANA 1:1-5)

'Hapo mwanzo kulikuwapo Neno, naye Neno alikuwapo kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo, wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika. Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu. Nayo nuru yang'aa gizani, wala giza halikuiweza. '

(Yohana 1:1-5)

## Juma la 1: Yeye ndiye Neno

**Yohana 1:1-2** 'Hapo mwanzo kulikiwapo Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu.'
Msisitizo wa juma hili ni juu ya hali ya uungu ya Yesu na uwepo wake wa milele.

## Juma la 2: Yeye ndiye Muumba

**Yohana 1:3:** 'Vyote vilifanyika kwa huyo, wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika.'
Juma hili, tunaangalia kuhusu uwezo wa kuumba wa Yesu na mamlaka yake juu ya uumbaji wote, tukiangazia ukuu wake kabla ya uumbaji wote

## Juma la 3: Yeye ndiye Uzima

**Yohana 1:4:** 'Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu.'.
Juma hili, tunachunguza wajibu wa Yesu kama mtoaji na mhifadhi wa uzima, anayetoa maisha ya kiroho na ya milele kwa wote wanao mwamini yeye.

## Juma la 4: Yeye ndiye Nuru

**Yohana 1:5** 'Nayo nuru yang'aa gizani, wala giza halikuiweza.'
Juma hili, tunatazama jukumu la Yesu kama yeye anayeleta nuru...yeye ambaye hufukuza giza la dhambi.

## Siku ya Krismasi: Yeye ndiye Imanueli

**Yohana 1:14:** 'Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli.
Leo, tunasherehekea Mungu kufanyika mwili katika Yesu Kristo, akiangazia uwepo wa karibu wa Mungu kati yetu na ukamilishaji wa ahadi za Mungu kupitia kwa kuzaliwa kwa Yesu.



'Hapo mwanzo kulikuwapo Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu.' (Yohana 1:1-2).

# Yeye ndiye Neno

Yohana 1:1-2, Yohana 1:11 na Yohana 8:58

'Hapo mwanzo kulikuwapo Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu.' (Yohana 1:1-2).

Tunapoingia Ujio, tukisubiri na kujiandaa kusherehekea kuzaliwa kwa Yesu, tukiiandaa mioyo yetu kwa ajili ya Krismasi, maneno ya Mtakatifu Yohana 1:1-2 yanatutangazia hali ya uungu na uwepo wa milele wa Yesu, aliyekuja 'kusimamisha hema lake' kati yetu.

Wayahudi walikuwa wanasubiri Masihi aje. Na hatimaye alipokuja, vile vile kama alivyotabiri, hawakumtambua Yesu kama Masihi: 'Alikuja kwake wala walio wake hawakumpokea.'(Yohana 1:11).

Tunapoangalia Injili nne zinavyomtambulisha Yesu, zile za kwanza tatu kila moja inamweka Yesu katika hali ya historia. Mathayo anaanza na orodha ndefu ya vizazi, na anamuunganisha Yesu na Mfalme Daudi na kumrudia Ibrahimu. Marko anamtambulisha Yesu kupitia kwa mahubiri ya Yohana Mbatizaji. Luka anakwenda mbali kidogo nyuma na Elizabeti na Zakaria na utabiri wa kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji. Lakini Yohana ni wa kipekee katika kumtambulisha Yesu kwetu.

Anatupeleka nyuma mbali iwezekanavyo sisi kufikiri. Mwanzo, kabla ya uumbaji wa dunia: 'Hapo mwanzo kulikuwapo Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu.'

Yohana anatupeleka nyuma kupita uumbaji kutukumbusha kwamba Yesu amekuwa Mungu Mwana kutoka milele, kwamba alikuwepo hata kabla ya kuzaliwa kwake, na kwamba anafanana na Mungu Baba.

Twamwona Yesu kama Neno la Milele, aliyekuwako toka mwanzo, sio kwa sababu alikuwa na mwanzo kama kiumbe, bali kwa sababu yeye ni wa milele. Yeye ni Mungu naye ni Mungu pamoja nasi. Katika Yohana 8:58, Yohana anarekodi maneno ya Yesu mwenyewe; 'Kabla ya Ibrahimu kuwepo, Nilikuwepo.'

Neno la Milele, aliyekuwa na Mungu naye alikuwa Mungu, alichagua kuingia katika dunia yetu kama mtoto asiyejiweza. Yeye, Neno, alisema na dunia ikawepo. Alikuja kuishi kati yetu ili awe mmoja wetu.

Kamishena Keith Conrad

# Na kwa hiyo, tunaposafiri katika Ujio, ni nini ambacho Yesu, ambaye ni Neno aliyesema tu dunia ikaumbika, anaweza kusema katika maisha yako katika majira haya?

Mpendwa Mungu, tunaingia katika majira haya ya Ujio tukisubiri kusherehekea ujio wa Mwanao wa milele duniani kwetu. Tunasimama tukiwa tunashangazwa na wewe. Tunakushukuru, Yesu, uliye - Mimi Ndiye, Alfa na Omega, kwa ajili ya upendo wako usio na masharti na kwa kuja kuishi pamoja nasi. Tusogeze karibu nawe majira haya ya Ujio. Twaomba tujazwe kuabudu na sifa kwako Krismasi hii tunaposherehekea upendo wako wa milele kwetu.

Amina.



‘Vyote vilifanyika kwa huyo,wala pasipo huyo
hakikufanyika cho chote kilichofanyika.’(Yohana 1:3).

# Yeye ndiye Muumba

Yohana 1:3

'Vyote vilifanyika kwa huyo,wala pasipo huyo hakikufanyika cho chote kilichofanyika.'(Yohana 1:3).

Moja ya kumbukumbu zangu za Krismasi ni wakati nilisimama na mama yangu, tukiangalia mapambo ya Krismasi katika dirisha kubwa. Maonyesho hayo ya ajabu yalitengenezwa kutokana na vifaa vilivyopatikana wakati huo: ubao, karatasi ya gundi, gundi, na taa kidogo. Bali kila dirisha liliwakilisha kitabu cha hadithi ya furaha ya majira.

Mapambo ya leo yanashangaza na ni yenye mchanganyiko wa ubunifu wa muziki, taa, na roboti. Waundaji wa uwakilishi wa kipekee wa karne ya 21 wana karama ya ubunifu na uwezo wa kuendesha miundo iliyowekwa inayofafanua.

Hata hivyo, hakuna uumbaji wa mwanadamu unaoweza kuanza kugusa uumbaji wa Mungu. Katika Injili ya Yohana, tunakutana na ufunuo mzito: Yesu sio tu ni Mwokozi wa ulimwengu, bali vile vile ni Muumba wa vitu vyote.

Ujumbe wa Krismasi ni Muumba anafanyika aliyeumbwa. Muumba aliingia katika uumbaji wake, akiivaa hali ya mwanadamu, jambo la ajabu kuu.

Krismasi hii, tunakiri Zawadi ya kweli ya Krismasi – kuzaliwa kwa Yesu Kristo.

Majira haya, tunaweza kufurahia maonyesho na mapambo ya kipekee ya Krismasi, hebu tukumbuke na tutafakari kuhusu yeye ambaye aliumba nyota na akaleta uzima, uzima tele duniani hapa, Yesu. Yesu muumba, anatualika tumtizame Yeye, sio kama onyesho katika dirisha dukani linalokamata fikra zetu, bali kama Mkombozi na Rafiki.

Kamishena Kenneth Maynor

# Nazingatia nini majira ya Krismasi hii na hii inaonyesha namna gani imani yenye ujasiri?

Mungu Baba, nakutukuza kwa uaminifu wako toka kizazi hadi kizazi. Neema, nguvu na upendo wako vyaonekana wazi katika majira haya kupitia kwa mwana wako, Yesu Kristo. Yaweke macho yangu yamzingatie Yesu – onyesho kuu sana la upendo, aliyeingia kwa unyenyekevu katika uumbaji wake ili atukomboe.

Amina.



‘Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao
ule uzima ulikuwa nuru ya watu.’
(Yohana 1:4).

# Yeye ndiye Uzima

Yohana 1:4, 1 Mambo ya Nyakati 16:34 na Luka 3:4

'Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu.' (Yohana 1:4).

Mwanzo wangu ulikuwa katikati au huenda ulikuwa mwishoni. Kabla sijaja, tayari nilikuwepo. Baada yangu, nitakuwepo.

Mimi ni sehemu ya picha kubwa. Ya kila kitu. Mtiririko wa mpango wa Mungu. Ndivyo yalivyo maisha yetu kutoka katika mtazamo wa milele, mtazamo wetu unapopanuka, na mawazo yetu kwenda kufikiria yote ya muda na nafasi. Tunaweza kuona jinsi malezi ya Mungu kwetu yameenda zaidi kuliko tunavyoweza kufikiria katika maisha yetu ya kila siku.

Yohana anaandika,'Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu (Yohana 1:4). Umilele wa Mungu unajumuisha wako na wangu sasa, jambo linalotupa sisi mahali imara pa ukamilifu pa kuanzia tunapopahitaji kila siku. Lakini nalo vile vile ni kubwa zaidi ya tunavyoweza kuhesabu au kuelewa. Halina mwisho. Halina kikomo.

Katika Yesu, Mungu anasogelea 'wanadamu wote'. Katika hali zote mbalimbali, mazingira, desturi au nyakati, Yeye anakuwa uzima, kwa kila mmoja. Kwa sababu 'fadhili zake ni za milele'(1 Mambo ya Nyakati 16:34).

Katika sehemu mbalimbali duniani, tunaweza tukawa na mila mbalimbali za Ujio. Katika mila yetu ya Kiswidishi, Jumapili ya tatu katika Ujio inamhusu Yohana Mbatizaji tu na ujumbe wa Kristo anayekuja. Sauti ya mtu aliaye nyikani, 'Itengenezeni njia ya Bwana, yanyoosheni mapito yake' (Luka 3:4).

Nami nafikiria kuhusu 'nyikani' ndani ya jamii yangu mwenyewe na majirani. Mahali ambapo watu wenye kuchoshwa wakati wa ujio wanahitaji kusikia kwamba kuna uzima. Katika ukamilifu wake. Kwa ajili ya kila mmoja. Vile vile kwa watu ambao hatuwaelewi au hata hatuwataki. Nuru ya wanadamu wote. Yesu. Nami nasikia msukumo wa kwenda 'nyikani' kuzunguka nyuma mahali watu wamechoshwa wanahitaji nuru katika handaki na kushirikishwa habari. Kuelezea hadithi kuu ya uzima tumaini, maana na kusudi tulilopewa katika Yesu. Ujumbe wa milele. Kwa ajili ya kila kizazi.

Kamishena Eva Kleman

# Ni kwa njia ipi mimi nakumbatia maisha ya Yesu katika mazingira yangu binafsi? Kuna jambo ambalo nataka kuwa tofauti, kama ndivyo, mpango wangu ni upi wa kulipata hilo?

Mungu, nasikia kizunguzungu. Je, kweli unamaanisha msamaha wako ni wa milele? Faraja yako haina kikomo? Majibu yako na uvumilivu wako hauchoki? Nasimama nikiwa nimeishiwa maneno na nashangazwa. Mimi ni sehemu...hata pungufu kuliko sehemu ya darubini, lakini bado napendwa na kukubalika kikamilifu, sehemu ya milele ya Mungu, kwa wakati huu, nikiwa katika mchakato wa kupata? Nina kizunguzungu cha shukrani! Nisaidie nipate njia ya kumshirikisha mwengine habari hii kuu leo. Nisaidie niipate sehemu yangu 'nyikani' niandae njia kwa ajili yako!

Amina



‘Nayo Nuru yang’aa gizani, wala giza halikuiweza.’. (Yohana 1:5)

# Yeye ndiye Nuru

Yohana 1:5 na Yohana 8:12

'Nayo Nuru yang'aa gizani, wala giza halikuiweza.'. (Yohana 1:5)

Tunapokuwa katika nyumba yenye giza na tukasikia kelele tusiyoitambua, kwa hisia tu sisi huwasha taa ili tuweze kuona na tuonekane. Nuru huangaza kwenye giza na hutusaidia tuone kila kitu wazi. Inazungumzia kuhusu usalama na uhakika, hekima na uelewa.

Nuru ina thamani safi sana, na yakuvutia. Inadhihirisha wema, kweli na utakatifu. Palipo na nuru, pana uzima. Palipo na nuru, giza haliwezi kudumu hapo.

Katika dunia hii, kuna giza jingi mno. Kuna dhambi na kuna uovu. Kila moyo wa mwanadamu unamenyana na vifungo vya dhambi, pamoja na moyo wa majivuno, mifumo ya mawazo yasiyo bora, na dhambi za tabia zinazoonekana kuwa ngumu kuachana nazo.

Lakini nuru ina uwezo na inaweza kufika mbali. Hakuna kitu wala mahali penye giza nene nuru ishindwe kuangaza.

Yesu alisema: '...Mimi ndimi nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima.' (Yohana 8:12).

Yesu ndiye aletaye nuru, yeye afukuzaye giza la dhambi kutoka kwa wale wanaomfuata. Yeye atuletaye kwenye nuru, aangazaye hatua yetu inayofuata na kutuonyesha njia. Yeye ndiye nuru ya ulimwengu.

Kama wafuasi wake Yesu, waliojazwa Roho Mtakatifu, tunaweza kuangaza nuru yake kwenye giza la dunia hii kupitia kwa maneno yetu na matendo yetu, tukiwasaidia wengine waone na waje nao wamfahamu yeye vile vile.

Kamishena John Kumar na Mani Kumari Dasari

# Ina maana gani kwako kwamba Yesu ni nuru? Ulifikaje kutambua nuru hii kuu? Nuru ya Yesu imefukuza namna gani giza litoke maishani mwako?

Mpendwa Bwana, asante kutuonyesha nuru yako na kutusaidia tutembee katika nuru yako. Tafadhali tusaidie tuangaze nuru hii na tuwaongoze wengine watoke kwenye giza waingie kwenye nuru.
Katika jina la Yesu naomba.

Amina



'Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli. ' (Yohana 1:14).

# Yeye ndiye Imanueli

Yohana 1:14, Mathayo 1:18-25, Isaya 7:14 na 2 Wakorintho 9:15

'Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli. ' (Yohana 1:14).

Ni Krismasi nasi tuna mengi ya kusherehekea!

Mungu yuko pamoja nasi – Yeye ndiye Imanueli.

Katika Yohana 1:14, twasoma kwamba 'Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu...' Tafsiri nyingine ya Biblia ya (The New Christian Version) kifungu hicho hicho inasema hivi: 'Neno likawa mwanadamu na akaishi kati yetu.'

Mungu akawa mwanadamu – mwili na damu. Kwa miaka thelathini na mitatu aliishi kama mwanadamu duniani, anayasikia yote ambayo wewe na mimi tunayasikia. Wanafunzi wa mwanzo walimuona na wakasikia kutoka kwenye mdomo wake yale aliyotaka kufundisha. Alikuwa wa kweli na binafsi, hakuwa wa kudhania na wa kutoka kijijini, hakuwa wa mbali au asiyejali.

Huyu ndiye Mungu wetu wa milele, awezaye kuwafikia wanadamu na hayuko mbali nasi watu wa kawaida. Huyu ndiye Mungu wetu wa milele, yeye ambaye inawezekana kumgusa, mwenye uso wenye hali ya mwanadamu hapa na sasa. Kuzaliwa huku kwa Yesu, ni utimilifu wa unabii uliotamkwa mapema na Isaya miaka mamia kabla. Mungu amekuwa mwanadamu.!

Inaonekana kuwa vigumu kwetu kufahamu ukubwa wa zawadi kwa kila mmoja wetu. Kufahamu kikamilifu kiwango cha neema hii, upendo huu kwa wanadamu. Mungu yuko pamoja nasi.

Hata leo, watu wanapopambana kuelewa Mungu ni nani na Mungu yukoje, tuna uhakika kupitia kwa neno lake na kupitia kwa uzoefu wetu naye kwamba tunaweza kumnyooshea kidole na kusema, 'Huyu hapa'!

Katika siku hii ya Krismasi, tunatambua ukweli kwamba Mungu yuko pamoja nasi – haijalishi tunakabiliana na nini, popote tulipo, uwepo wake upo pamoja nasi. Tunaposherehekea kuzaliwa kwa Mwokozi wetu, Imanueli, Mungu pamoja nasi, naomba tuungane na Mtume Paulo kutangaza:

'Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo!'
(2 Wakorintho 9:15)

Tunapokea zawadi ambayo hatungeweza kulipwa wala hatungeweza kustahili – ni zawadi kutoka kwa Mungu ya kupita kiasi namna gani.

Kamishena Wayne Maxwell

# Ni kwa njia zipi ukweli kwamba Mungu yuko pamoja nasi unakuhimiza na kubariki maisha yako?

Mungu Baba
Leo, tunaungana na Wakristo duniani kote kusherehekea kuzaliwa kwa Mwokozi wetu Yesu. Aliingia katika dunia yetu sio kama mwanadamu bali kama mwanadamu. Asante kwa zawadi hii isiyoweza kuelezeka. Tunakiri neema na upendo wako kwa kila mmoja wetu. Tusaidie kuishi kila siku tukitambua kwamba upo pamoja nasi na kwamba katika chochote tunachoweza kuwa tunakabiliana nacho, tutambue uwepo wako, nguvu na uwezo wako.

Amina

SPIRITUAL
LIFE DEVELOPMENT
INTERNATIONAL HEADQUARTERS

Images sourced from pexels.com